# MAELEZO YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHESHIMIWA JOACHIM LEONARD WANGABO WAKATI WA KUWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) KWENYE KIKAO CHA HALMASHAURI KUU YA CCM (M) TAREHE 12 OKTOBA, 2018

## 1.0 Utangulizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mkoa umeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015. Ilani hiyo inayo maelekezo mahsusi kwa Serikali tunapoelekea kujenga Uchumi wa Viwanda na Taifa lenye Uchumi wa kipato cha Katia. Aidha, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Serikali inaelekeza nguvu zake zote katika kuendelea kupambana na changamoto kubwa Nne (4) ambazo ni kupunguza umasikini; tatizo la Ajira hasa kwa vijana; Vita dhidi ya Rushwa na ubadhirifu wa mali za Umma na jukumu la kudumisha amani na utulivu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Taarifa hii inaeleza kwa ufupi utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 kwa kipindi kilichoishia Juni, 2018 kwa baadhi ya Sekta. Tathmini hii inafanywa katika mwaka wa pili na nusu wa kipindi cha kwanza cha Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano. Tathimini imebainisha kwamba utekelezaji wa Ilani ya CCM (2015) ambayo imebakiza karibu miaka miwili katika uhai wake ni wenye mafanikio makubwa.

## 2.0 Mafanikio yaliyopatikana

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mafanikio yamepatikana katika Sekta zote ambapo msukumo umewekwa katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Msingi wa kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 umetafsiriwa katika Sera za Kisekta na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Maudhui ya mpango huu ni "**Kujenga Uchumi wa Viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu".**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** vilevile Programu, Miradi Mipango na Mikakati mbalimbali ya Kisekta imeeendelea kutekelezwa kwa mafanikio makubwa. Hii ni pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

## 2.1 Pato la Mwananchi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Pato la Mwananchi katika Mkoa nalo limekuwa likiongezeka kutoka Shilingi 3,714,792 Mwaka 2016 hadi kufikia Shilingi 4,064,393 Mwaka 2017 kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa Mwezi Aprili, 2018 na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kipindi cha mwaka 2015/2016 mapato ya ndani kwa Halmashauri zote yalikuwa ni Tsh. 5,562,775,709 ya lengo ambalo ni Tsh. 6,319,833,660. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2017/2018 makusanyo yaliongezeka hadi kufikia Tsh. 6,983,565,000 ya lengo ambalo ni Tsh. 9,508,996,000.

Mchanganuo wa makusanyo ya mwaka 2017/2018 kwa kila Halmashauri ni kama ifuatavyo;

| Na. | Halmashauri | Makisio (Tsh) | Mapato halisi (Tsh) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sumbawanga DC | 2,394,825,000 | 2,143,573,781 | 90 |
| 2 | Nkasi DC | 2,299,602,000 | 2,065,890,879 | 90 |
| 3 | Kalambo | 2,219,532,000 | 1,408,478,771 | 63 |
| 4 | Sumbawanga MC | 2,595,037,000 | 1,365,621,669 | 53 |

Katika kipindi cha Mwaka 2018/2019 kuanzia Mwezi Julai hadi Septemba, 2018 makusanyo ni kama ifuatavyo;

| Na. | Halmashauri | Makisio (Tsh) | Mapato halisi (Tsh) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sumbawanga MC | 2,212,104,000.00 | 611,093,767.13 | 28% |
| 2 | Nkasi DC | 2,304,000,000.00 | 532,781,324.61 | 23% |
| 3 | Sumbawanga DC | 2,301,526,000.00 | 311,374,402.44 | 14% |
| 4 | Kalambo DC | 2,000,000,000.00 | 191,531,828.16 | 10% |
| | **Jumla** | **8,817,630,000.00** | **1,646,781,322.34** | **18%** |

**Mpango wa kunusuru Kaya Masikini (TASAF)**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kipindi cha mwaka 2015/2016 hadi mwaka 2017/2018 jumla ya fedha kiasi cha Tsh. 1.45 bilioni zilitolewa na Serikali kwa ajili ya kaya masikini na Miradi ya ujenzi (Public Work Program-PWP). Hivyo, Serikali imeendelea kuwasaidia Wananchi wake hasa wale masikini ili kujikwamua kiuchumi.

## 2.2 Huduma za Kijamii

### 2.2.1 Afya

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Huduma za Jamii zikiwemo Afya na Elimu zimeendelea kuimarika. Hadi sasa Serikali imetoa jumla ya **Shilingi Bilioni 4.1** zilizotumika kujenga na kukarabati vituo vya Afya vifuatavyo:-

(i) Kituo cha Afya Mazwi - Shilingi 500,000,000/=
(ii) Kituo cha Afya Katumba Azimio - Shilingi 400,000,000/=
(iii) Kituo cha Afya Nkomolo - Shilingi 500,000,000/=
(iv) Kituo cha Afya Kirando - Shilingi 400,000,000/=
(v) Kituo cha Afya Wampembe- Shilingi 400,000,000/=
(vi) Kituo cha Afya Milepa - Shilingi 400,000,000/=
(vii) Kituo cha Afya Legezamwendo - Shilingi 700,000,000/=
(viii) Kituo cha Afya Mwimbi - Shilingi 400,000,000/=
(ix) Kituo cha Afya Kanyezi - Shilingi 400,000,000/=

Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya kwa kuhakikisha kila Wilaya inakuwa na Hospitali ya Wilaya. Kwa Mkoa wetu zitajengwa Hospitali tatu kwa maana Halmashauri ya Sumbawanga Vijiji (Mtowisa), Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi (Eneo la Mkangale- Namanyere) na Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo eneo la Matai. Hospitali zote hizi zimetengewa kiasi cha Shilingi 1.5 bilioni kila moja na tayari kila Halmashauri imeshapokea kiasi cha Shilingi 500,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Aidha, ili kuendelea kuboresha huduma za afya katika ngazi za Vijiji Mkoa umefanikiwa kuongeza Zahanati kutoka 181 mwaka

2015 hadi 200 mwaka 2018. Hata hivyo ujenzi wa maboma ya Zahanati 60 unaendelea katika Mkoa wetu.

**Upatikanaji wa dawa.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** hali ya upatikanaji wa dawa ndani ya Mkoa imeimarika kutoka asilimia 67 mwaka 2017 hadi asilimia 85 mwaka 2018. Aidha, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya dawa kutoka Tsh. 1,251,961,739.00 kwa mwaka 2015 hadi kufikia Tsh. 2,991,860,620.69 mwaka 2018.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mkoa unaendelea kuhimiza Halmashauri kuimarisha vyanzo vya makusanyo ya ndani ili kuwa na fedha za kutosha kununua dawa. Vyanzo hivyo ni pamoja na fedha za ruzuku ya dawa na vifaa kutoka Serikali kuu kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD), fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo kupitia mfuko wa pamoja wa afya (HBF) fedha zinazotokana na mifuko ya uchangiaji wa huduma za afya na sehemu ya fedha ya makusanyo ya ndani (*Councils' Own Source Collections*). Aidha, Mshitiri (*Prime Vendor*) ameshapatikana na mapendekezo yameshawasilishwa kwa Katibu wa Bodi ya zabuni ya Mkoa kwa ajili ya taratibu za kumpatia mkataba, hivyo kuongeza upatikanaji wa dawa nje ya Bohari Kuu ya Dawa.

### 2.2.2 Sekta ya Elimu

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa upande wa Sekta ya Elimu, azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha kila Mtoto anayestahili kupata Elimu Msingi (*Basic Education*) anapata Elimu hiyo. Mpango wa Serikali wa Elimu Msingi bila malipo umekuwa na mafanikio makubwa. Mafanikio hayo ni pamoja na;-

(i) Asilimia ya uandikishaji wa darasa la kwanza umeongezeka kutoka 40,404 mwaka 2016 hadi 50,887 sawa na ongezeko la 26% mwaka 2018.

(ii) Idadi ya Wanafunzi wa kidato cha **I-VI** imeongezeka kutoka 25,241 mwaka 2016 hadi kufikia 33,723 mwaka 2018. Hii ni sawa na ongezeko la 34%.

(iii) Idadi ya shule zenye Kidato cha Tano na Sita zimeongezeka kutoka 10 (Mwaka 2016) hadi kufikia 15 (Mwaka 2018). Hii ni sawa na ongezeko la 50%.

(iv) Kipindi cha Mwaka 2017-2018 Serikali imetoa kwa Mkoa Jumla ya Shilingi **5,114,012,715.00** za elimu bila malipo kwa shule za Msingi na Sekondari ikiwa ni fedha kwa ajili ya Ruzuku (*Capitation Grant*), fedha ya chakula, posho ya waratibu elimu Kata, posho ya walimu wakuu, wakuu wa shule na fidia ya ada.

**Mafanikio Kitaaluma:**

**Matokeo ya Mitihani Mwaka 2017/2018**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mkoa umeendelea kusimamia suala la Elimu kikamilifu. Aidha, katika upimaji wa Mitihani ya kitaifa matokeo ya ufaulu yamekuwa yakiongezeka kama ifuatavyo;

**(i) Matokeo ya darasa la Nne**

Matokeo ya mtihani wa upimaji kwa Darasa la Nne yameendelea kuimarika kutoka ufaulu wa aslimia 88.00 kwa mwaka 2016 hadi asilimia 89.11 kwa mwaka 2017 .

**(ii) Matokeo ya Darasa la Saba, 2017**

Matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi yanaonesha kupanda kwa ufaulu wa wanafunzi kutoka ufaulu wa 66% kwa mwaka 2016 hadi 68.05% kwa mwaka 2017. Kulingana na Tathmini ya mtihani wa utimilifu ufaulu unatarajia kuongezeka hadi kufikia asilimia 78% kwa mwaka 2018.

Idadi ya Wanafunzi waliofaulu 12,867 wote walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2018. Kati yao Wanafunzi 54 shule za bweni na 12,813 shule za kutwa. Wanafunzi hao wote walipatiwa nafasi za kuendelea na masomo.

**(iii) Matokeo ya kidato cha pili**

Katika mtihani wa upimaji Kidato cha Pili mwaka, 2017, ufaulu wa wanafunzi uliongezeka kutoka asilimia 87.6 mwaka 2016 hadi asilimia 92.08 kwa mwaka 2017.

**(iv) Matokeo ya kidato cha Nne**

Matokeo ya mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2016, Mkoa ulishika nafasi ya 12 kitaifa kati ya Mikoa 31 ukilinganisha na mwaka 2017 ambapo Mkoa ulishika nafasi ya 13. Aidha Jitihada za ufundishaji, ufuatiliaji na usimamizi zimefanyika ili kwa mwaka 2018 Mkoa uwe katika nafasi nzuri zaidi kitaifa.

**(v) Matokeo ya kidato cha Sita**

Matokeo ya mtihani wa Kidato cha Sita mwaka 2017 Mkoa ulishika nafasi ya 8 kitaifa kati ya Mikoa 29

ukilinganisha na mwaka 2018 ambapo Mkoa ulishika nafasi ya 13. Aidha, jitihada za ufundishaji, ufuatiliaji na usimamizi zinaendelea kufanyika ili kwa mwaka 2019 Mkoa uweze kushika nafasi nzuri zaidi kitaifa ukilinganisha na mwaka huu.

**Utekelezaji wa miundombinu ya elimu Mkoa**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali inaendelea na jitihada za kuboresha miundombinu mbalimbali ya elimu kama ifuatavyo;

**(i) Miundo mbinu ya Maabara**

Katika kipindi cha mwaka 2015 tulikuwa na maabara 24, na kwa mwaka 2018 maabara zimeongezeka hadi kufikia maabara 31. Aidha, maabara 177 zinaendelea kujengwa katika Mkoa wetu ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

**(ii) Vyumba vya Madarasa**

Katika kipindi cha mwaka 2015 Vyumba vya madarasa vilivyokuwepo kwa shule za msingi na Sekondari ni 3,140 na kwa mwaka huu wa 2018 vyumba vya madarasa vimeongezeka hadi kufikia 3,329.

**(iii) Nyumba za Walimu:**

Katika kipindi cha mwaka 2015 nyumba za walimu wa shule za msingi na Sekondari zilikuwa ni 1,955 na kwa mwaka 2018 zimeongezeka hadi kufikia nyumba 2,124.Ongezeko hili ni jitihada za serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu kwa walimu.

**(iv) Matundu ya Vyoo**

Katika kipindi cha mwaka 2015 matundu ya vyoo yalikuwepo ni 4,391 na kufikia mwaka 2018 matundu ya vyoo yameongezeka kufikia 5,438.

**(v) Madawati:**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha sekta ya elimu kwa kuhakikisha madawati yanatengenezwa mashuleni. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2015/2016 tulikuwa na madawati 37,311 kwa shule za msingi, meza 21,757 na viti 22,093 kwa shule za Sekondari. Aidha, kwa mwaka 2018 madawati yameongezeka kufikia 80,501 kwa shule za msingi, meza na viti 33,686 kwa sekondari kufikia mwaka huu 2018.

**(vi) Mimba kwa Wanafunzi**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** tatizo la mimba kwa wanafunzi wanaosoma Elimu ya Msingi na Sekondari ni kubwa. Kuanzia Julai 2017 hadi Mei, 2018 jumla ya wanafunzi 121 wamepata ujauzito, kati ya hao wanafunzi wa Elimu ya Msingi ni 46 na wa Elimu ya Sekondari ni 75. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na Watendaji wa Kata kufikisha kesi hizo Polisi na Mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi. Mpaka sasa matukio yote 121 yameripotiwa Polisi kwa ajili ya hatua za kisheria.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili kukabiliana na tatizo la mimba mikakati mbalimbali imewekwa ikiwemo ifuatayo;

(i) Kutoa elimu kwa jamii pamoja na wanafunzi hasa wakike juu ya hasara za kupata mimba wakati bado ni

mwanafunzi ili waone umuhimu wa kuacha tabia hiyo.

(ii) Ujenzi wa shule shikizi za msingi pamoja na kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na shule ya msingi. Shule shikizi 13 zimejengwa na zinatumika. Aidha, katika kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na shule za msigi, hadi sasa tunayo maboma 372 kwa shule za msingi na maboma ya vyumba vya madarasa 30 kwa shule za Sekondari ambayo tunaendelea na jitihada za kuhakikisha yanakamilika kwa wakati ili wanafunzi hawa waondokane na adha hiyo. Aidha, katika jitihada hizi nipende kuwashukuru wadau mbalimbali hasa wananchi wenyewe, serikali na Chama Cha Mapinduzi kwa michango yao ya namna moja au nyingine iliyofanikisha ujenzi wa miundombinu ya madarasa.

(iii) Chakula kwa wanafunzi ambapo hamasa kwa wazazi na kamati za shule imetolewa kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula shuleni.

(iv) Ujenzi wa Hosteli za wasichana kwenye shule za Sekondari za Kata ambapo jumla ya Hosteli 54 zimejengwa.

(v) Kushirikiana na mahakama ili wahusika wanaojihusisha na kuwapa mimba wanafunzi wachukuliwe adhabu kali kisheria.

**Ujenzi wa chuo cha VETA Sumbawanga**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** tarehe 31/08/2018 VETA Makao Makuu Dar es Salaam, VETA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa tulifanya hafla fupi ya

kumkabidhi Mkandarasi TENDER INTERNATIONAL kiwanja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Chuo Cha Ufundi Stadi (VETA) katika Manispaa ya Sumbawanga pamoja na Mkandarasi, Mshauri Elekezi (Consultant) Sky Architect Consultancy Ltd.
Eneo hilo ambalo VETA itajengwa lipo Kashai (MUVA) katika Manispaa ya Sumbawanga na lina ukubwa wa 95,934 sq M Plot 1 Block 'A' (LD) chenye hati Namba 44102-MBYLR iliyotolewa tarehe 5 Machi, 2018.

Mradi unategemewa kukamilika ndani ya miezi 12 (kuanzia tarehe ya makabidhiano). Aidha, gharama za ujenzi za mradi huu ni Tsh. 10,700,488,940.05. Ujenzi ukikamilika chuo kitaweza kuchukua wanafunzi 900 wa kozi ndefu na 600 wa kozi fupi hivyo, kitakuwa na uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 1,500.

**Hali ya upatikanaji wa Maji mkoani.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kuboresha huduma za Maji katika Mkoa. Katika kipindi cha Mwaka 2015 upatikanaji wa maji ndani ya Mkoa ulikuwa ni asilimia 45 aidha, kufikia mwaka huu 2018 hali ya upatikanaji wa maji umeongezeka hadi kufikia asilimia 53.5.

Katika kuhakikisha huduma ya maji inaongezeka, Serikali kupitia Wizara ya Maji imetenga kiasi cha shilingi **5,686,194,000/=** kwa mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa miradi ya maji na kampeni ya usafi wa mazingira.

## 2.3 Miundombinu ya Barabara

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kwa upande wa Miundombinu, Serikali imeendelea kujenga na kukarabati barabara pamoja na Miundombinu mingine. Barabara mpya zilizoanza kujengwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne zimekamilika. Barabara hizo ni zifuatazo:-

(i) Sumbawanga - Chala – Kanazi (Km 75)

(ii) Kanazi -Kizi - Kibaoni (Km 76.6)

(iii) Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (Km. 112) (Ujenzi umefikia asilimia 76)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kuboresha miundombinu ya barabara katika Mkoa wetu ikiwemo ujenzi wa daraja kubwa lenye urefu wa mita 84 linajengwa eneo la Kilyamatundu/ Kamsamba katika Mto Momba kwa gharama ya Shilingi 17.7 Bilioni. Ujenzi wa Daraja hili ulianza tarehe 1 Agosti, 2017 na lilipaswa kukamilika baada ya miezi 13 yani 31 Agosti, 2018. Aidha, kutokana na changamoto ya mafuriko ya Mto Momba wakati wa mvua za masika kazi za ujenzi ziliahirishwa hivyo, ujenzi huo sasa utakamilika Mwezi Februari, 2019. Hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 65 ambapo tayari mkandarasi amekwishajenga nguzo (*pivers*) mbili na kingo (abutments) mbili za upande wa Kilyamatundu na Kamsamba pia ujenzi wa beams na sakafu (*deck slab*) umekamilika. Kukamilika kwa Daraja hili kutaongeza fursa za kiuchumi katika eneo la Bonde la Ziwa Rukwa hivyo

kuendelea kuifungua Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla.

## 3.0 Ushirikishwaji wa Wadau

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 yametokana na mchango wa wadau mbalimbali Mkoani Rukwa. Wadau hao ni pamoja na:-

(i) Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa
(ii) Ofisi za Wakuu wa Wilaya
(iii) Mamlaka za Serikali za Mitaa
(iv) Wananchi.
(v) Viongozi wa CCM wa ngazi mbalimbali.
(vi) Sekta Binafsi
(vii) Taasisi Wakala na Mashirika ya Umma
(viii) Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs)
(ix) Mashirika ya Dini
(x) Vyombo vya Habari

## 4.0 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Taarifa itakayowasilishwainaSura Nane (8) ambazo zinaeleza mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 katika maeneo yafuatayo:-

(i) Ukuaji wa Uchumi na Sekta ya Fedha
(ii) Huduma za Uzalishajimali
(iii) Huduma za Kiuchumi
(iv) Huduma za Jamiii
(v) Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
(vi) Mafanikio katika maeneo mengine ya kipaumbele

**5.0 Hitimisho**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wananchi wameendelea kuiamini Serikali yao na kuishi kwa Amani na utulivu Mkoani Rukwa. Jambo hili limesaidia Serikali katika Mkoa kutekeleza kwa mafanikio Ilani na ahadi zilizotolewa kwa wananchi wakati wa Kampeni za uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Mafanikio haya yanayotoa taswira sahihi ya uongozi mahiri wa Kiongozi Mkuu wa Nchi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM Taifa. Aidha, uongozi huo umeendelea kuweka na kuimarisha mazingira mazuri ya **Sera, Mikakati, Sheria, Kanuni na Taratibu za kusimamia na kuendesha shughuli za Serikali kwa kuzingatia Utawala Bora.** Kwa ujumla kasi ya utekekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na ahadi za Mgombea Urais alizotoa mkoani Rukwa inakwenda vizuri na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho yanaonekana. Serikali katika Ngazi ya Mkoa kwa kuwashirikisha wadau wote itaendelea kuhakikisha kuwa kasi ya utekelezaji inaongezeka na miradi iliyoanza kutekelezwa mfano; miradi ya maji, umeme kupitia REA inamalizika kwa wakati na Wananchi kufahamishwa bayana yale ambayo Serikali inatekeleza kwa manufaa yao.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Nimeambatana na Mtaalam kutoka Ofisi yangu. Kwa kuzingatia mwongozo wako yupo tayari kutoa maelezo na ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2015 kwa rejea ya ibara mbalimbali za kisekta.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Naomba kuwasilisha.